

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Simu Na: +255(026) 2502170
Nukushi: +255(026) 2502078
Barua Pepe: ras@singida.go.tz
Tovuti: <http://www.singida.go.tz>



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida,
Mtaa wa Bomani,
S.L.P 05,
SINGIDA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. GH. 32/129/02/128

04 Aprili, 2024

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa,
Singida.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri za Wilaya,
Ikungi, Iramba, Manyoni na Mkalama.

**Yah: KLINIKI ZA KUZUIA NA KUPAMBANA NA SARATANI YA NGOZI KWA WATU
WENYE UALBINO KWA MWAKA 2024**

Husika na somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imepokea barua Kumb.Na.CB.161/352/01 ya tarehe 29 Disemba, 2023 kuhusu somo tajwa hapo juu. OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Shirika la Standing Voice Tanzania, Regional Dermatology Training Centre (RDTC KCMC – MOSHI) na Tanzania Albinism Society (TS) wataendesha Kliniki ya macho na kufanya uchunguzi wa Saratani ya ngozi kwa watu wote wenye Ualbino kwenye Halmashauri zenu.
3. Kliniki hii ni ya bure kwa watu wote wenye Ualbino. Aidha, wagonjwa watakaobainika kuwa na dalili zozote zenye uhusiano na Saratani ya ngozi watapatiwa matibabu kwa njia ya cryotherapy na kwa wale ambao watahitaji matibabu zaidi watapewa rufaa kwenda KCMC, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili au Ocean Road.
4. Kwa barua hii, nawataarifu uwepo wa zoezi hili muhimu linalotarajiwa kuanza tarehe **09 - 14 Aprili, 2024**, hivyo mnaombwa kuandaa eneo la utoaji wa huduma hizi. Ratiba ya zoezi hili imeambatishwa.
5. Ninashukuru kwa ushirikiano.


V.P. Kiwango

Kny:- **KATIBU TAWALA WA MKOA**

Nakala:- Makatibu Tawala wa Wilaya,
MKOA WA SINGIDA

RATIBA YA KLINIKI YA NGOZI KWA WATU WENYE UALBINO

Halmashauri	Eneo	Tarehe
Iramba DC	Iramba DH	09/04/2024
Mkalama DC	Mkalama DH	10/04/2024
Manyoni DC	Manyoni DH	11/04/2024
Singida MC	Singida MC	12/04/2024
	Minor Surgery	13/04/2024
Ikungi DC	Ikungi DH	14/04/2024